**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**Ofisi ya Makamu wa Rais**

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## KUVUNJA BODI YA BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC), MABADILIKO YA UONGOZI NEMC NA HATUA ZA KUHARAKISHA NA KURAHISISHA MCHAKATO WA KUPATA CHETI CHA EIA KWA WAWEKEZAJI WA VIWANDA

**Ndugu wananchi.**

Kama mnavyofahamu Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ni muhimu sana katika kuhakikisha ustawi wa mazingira na mustakabali wa maendeleo endelevu ya nchi yetu. Tunapoelekea kuwa nchi ya uchumi wa viwanda, usimamizi wa mazingira lazima uwe **imara na urahisishe na kuharakisha utekelezaji wa ujenzi wa viwanda, miradi mbalimbali na uwekezaji katika sekta zote ili kwenda kwa kasi na weledi unaotakiwa.**

Utendaji wa NEMC umekuwa ukilegalega sana na umekuwa hauridhishi. Siku za hivi karibuni pamekuwepo na malalamiko mengi kutoka kwa wawekezaji wa ndani na nje na wananchi wengi pia. Malalamiko hasa yamehusu mambo yafuatayo:-

1. Ucheleweshaji na urasimu usiokuwa wa lazima katika mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (EIA);
2. Tuhuma za rushwa katika mchakato wa ukaguzi na tathmini ya athari kwa mazingira;
3. Mazingira ya rushwa katika kutengeneza vyeti ambavyo havijafuata mchakato stahiki;
4. Kutokuwa na lugha nzuri kwa wateja na kuwatisha ili watoe chochote;
5. Kutumia makampuni binafsi ya watumishi wa NEMC kufanya kazi za ukaguzi/uhakiki wa ndani ya NEMC kwa kisingizio cha kutokuwa na watumishi wa kutosha;
6. Kuwaelekeza wawekezaji kwa makampuni ya kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (EIA) ambayo yanamilikiwa au yenye ubia na watumishi wa NEMC hivyo bila kujali mgongano wa kimaslahi, mambo ambavyo hayaruhusiwi kwenye utumishi wa umma;
7. Kuwarundikia maandiko ya miradi ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (EIA) watumishi wachache wakati wengine hawana kazi ili waelekeze miradi hii katika makampuni ambayo baadaye huwapatia malipo yasiyo halali. Baadhi ya wenye makampuni ambako miradi hii hupelekwa ni watumishi wa NEMC ambao wameacha au wameachishwa kazi.

Kwa kipindi kirefu, tumejitahidi kurekebisha hali hii na kumejitokeza nafuu lakini bado

hali haijafikia pale nilipotarajia. Nimefuatilia kwa karibu na kugundua kuwa matatizo mengi haya na mengine ya msingi yanasababishwa hasa na usimamizi usio imara wa Bodi na pia watendaji wakuu wa NEMC.

Kutokana na sababu hizi nimeamua kufanya yafuatayo:

1. Kulingana na mamlaka niliyonayo chini ya Sheria ya Mazingira kifungu cha 19 (2) nimeamua leo kutengua uteuzi wa wajumbe wote saba wa bodi ya NEMC ili baadaye niteue wajumbe wapya ambao wataenda na kasi na ari tunayoihitaji sasa katika kuelekea uchumi wa viwanda. Mwenyekiti wa Bodi, ambaye mamlaka yake ya uteuzi ni Mheshimiwa Rais, ataendelea kuwepo hadi Mheshimiwa Rais atakapoteua mwingine.

2. Tumemteua Dkt. Elikana Kalumanga, Mhadhiri katika Taasisi ya Usimamizi na Tathmini ya Rasilimali Asili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kuwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa NEMC hadi Mhe. Rais atakapoteua Mkurugenzi Mkuu.

Aidha, ili kuboresha utendaji wa NEMC tumefanya mabadiliko kadhaa ya Wakurugenzi na Wakuu wa Kanda za NEMC kama ifuatavyo: -

(a) Bwana Charles Wangwe, Mkurugenzi wa Fedha na Utawala wa NEMC amerejeshwa Wizara ya Fedha na Mipango mara moja kuanzia leo ambapo atapangiwa kazi kulingana na mahitaji ya Serikali. Kaimu Mkurugenzi wa Fedha na Utawala atakuwa Bwana Adam Minja kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais.

(b) Wakuu wa Kanda za NEMC wanadilishwa kama ifuatavyo: Bwana Jafari Chimgege, aliyekuwa Kanda ya Mashariki, sasa atakuwa Mkuu wa Kanda ya Kati - Dodoma; Bwana Goodlove Mwamsojo, aliyekuwa Mkuu wa Kanda ya Nyanda za Juu – Mbeya, sasa atakuwa Mkuu wa Kanda ya Mashariki – Dar es Salaam; Dkt. Ruth Rugwisha, aliyekuwa Mkuu wa Kurugenzi ya Ufuatiliaji na Uzingatiaji wa Sheria, sasa atakuwa Mkuu wa Kanda ya Ziwa – Mwanza; Bwana Dkt. Vedastus Makota, aliyekuwa Mkurugenzi wa Mawasiliano na Elimu kwa Umma, sasa atakuwa Mkuu wa Kanda ya Kusini - Mtwara; Bwana Joseph Kombe, aliyekuwa Mkuu wa Kurugenzi ya Utafiti na Mipango wa NEMC anakwenda kuwa Mkuu wa Kanda ya Kaskazini - Arusha, na Dkt. Menard Jangu, aliyekuwa Kanda hiyo anarudishwa Makao Makuu ya NEMC kuwa Kaimu Mkuu wa Kurugenzi ya Utafiti na Mipango. Bwana Jamal Baruti, aliyekuwa Mkuu wa Kanda ya Ziwa, anarudi Makao Makuu NEMC. Bwana Lewis Nzari aliyekuwa Mkuu wa Kanda ya Kusini – Mtwara, sasa anakuwa Mkuu wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini – Mbeya.

(c) Tumemteua Bi. Risper Koyi, kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, kuwa Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria NEMC kuchukua nafasi ya Bwana Wanjara Jandwa ambaye anahamishiwa Kanda ya Kati-Dodoma.

(d) Tumemteua Dkt. Yohana Mtoni, Afisa Mazingira Mkuu NEMC, kuwa Kaimu Mkuu wa Idara ya Ufuatiliaji na Uzingatiajiwa Sheria kuchukua nafasi ya Dkt. Ruth Rugwisha ambaye anakwenda kuwa Mkuu wa Kanda ya Ziwa - Mwanza.

(e) Tumemteua Bwana Carlos Mbuta, aliyekuwa Afisa Mawasiliano Mkuu wa NEMC, sasa atakuwa Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano na Elimu kwa Umma wa NEMC.

3. Pia tumewasimamisha kazi watumishi wa NEMC wafuatao wakati uchunguzi unafanyika kuhusu tuhuma zinazowakabili kwenye utendaji wao: Bwana Manchare Heche; Bwana Deus Katwale; Bwana Andrew Kalua na Bwana Benjamin Dotto; Wengine watafuatia wakati tukiendelea kupokea taarifa za ziada.

4. Hatua zote tulizotangaza za nidhamu na uhamisho zinaanza mara moja.

5. Nimeelekeza kwamba Wakuu wote wa Kanda wazingatie kwamba Sheria ya Mazingira na Kanuni zake zinazingatiwa kwa ukamilifu wake. Vilevile, tunaelekeza kwamba masharti ya kuhakikisha mchakato wa Tathimi ya Athari kwa Mazingira (EIA) na Ukaguzi wa Mazingira (EA) kwa maeneo yao unasimamiwa kwa kushirikisha maafisa mazingira wa halmashauri husika na usichukue muda zaidi ya ulioanishwa kwenye Sheria ya Mazingira. Liwe ni jukumu la Mkuu wa Kanda kuhakikisha hakuna mwekezaji ambaye hatajulishwa hitaji la Tathimi ya Athari kwa Mazingira (EIA) katika hatua za awali za mradi husika na kutoa kila ufafanuzi unaotakiwa katika muda wa siku moja.

6. Kufuatia maamuzi ya Bunge na maelekezo ya Mheshimiwa Rais kuhusu kuharakisha na kurahisisha mchakato wa Tathimi ya Athari kwa Mazingira (EIA), tunatangaza hatua zifuatazo:-

    a) Miradi yote inayohusu ujenzi wa viwanda, baada ya mwekezaji kuwasilisha taarifa hitaji la ujenzi wa kiwanda kwa NEMC, ruhusa ya ujenzi wa kiwanda itatolewa ndani ya siku tatu za siku za kazi wakati mchakato wa EIA unaendelea bila kuzuia wala kuchelewesha ujenzi wa kiwanda. Iwapo kutajitokeza changamoto, zitarekebishwa wakati wa mradi unaendelea na iwe ni sehemu ya "environmental management plan – EMP".

    b) Kutakuwa na Dawati Maalum la Miradi ya Viwanda pale NEMC na Ofisi ya Makamu wa Rais ili kushughulikia kwa haraka maswali ya masuala yote yanayohusu ujenzi wa viwanda.

    c) Maeneo yote yanayopangwa kujengwa viwanda, baada ya kujulikana, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na mamlaka nyingine, zitagharamia Tathmini ya Kimkakati ya Mazingira (TAMK) – *Strategic Environmental Assessment* (SEA). Suala hili litaondoa haja ya kila kiwanda kufanya EIA kamili. Viwanda vidogo vitakavyojengwa katika maeneo hayo maalum havitahitaji Cheti cha EIA labda kwa sababu maalum ambazo zitatolewa na NEMC, na Waziri lazima aridhie kwanza. Kwa msingi huo, tunasisitiza Wizara husika zitenge maeneo ya ujenzi wa viwanda ili sisi tuyafanyie Tathmini ya Mazingira ya pamoja kwa eneo lote.

    d) Miradi yote midogo na ya kati inayohusiana na viwanda vya kilimo na mifugo na uvuvi (small and medium scale agro processing industries) katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kilimo yatasamehewa gharama za kufanyiwa TAM. Taarifa za miradi hii zitatolewa kwa Afisa Mazingira wa eneo husika ili kuhakikisha wawekezaji wanasaidiwa kuzingatia kanuni bora za mazingira wakati wa utekelezaji wa miradi hii. Kama kuna haja ya baadhi ya miradi kufanyiwa tathmini wakati wa utekelezaji, fedha za kazi hiyo

zitatolewa na serikali kama sehemu ya OC.

e) Kuanzia sasa miradi itakayopelekwa NEMC kuombewa Cheti cha EIA ni ile ambayo tayari imefanyiwa kazi na washauri elekezi (consultants). Hapatakuwepo na haja ya kusajili mradi NEMC kwanza. NEMC itaweka maafisa katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na maeneo mengine muhimu ili kuhakikisha suala la kuwa na cheti cha mazingira linakuwa sehemu ya hatua za awali pale ambapo mwekezaji au mwenye mradi anapoanza kuomba vibali vingine. Aidha, utaratibu huu utatangazwa katika magazeti yote muhimu na vyombo vingine vya habari.

f) Nimeagiza NEMC wiki hii wafute watu binafsi na makampuni yote ya ushauri wa EIA (consultants) ambayo hayana sifa au yameshindwa kutekeleza kazi zao vizuri na watangaze kwenye magazeti yote muhimu orodha ya watu binafsi na makampuni ambayo yanaruhusiwa kufanya kazi kama washauri elekezi (consultants) katika masuala ya EIA. Orodha ionyeshe expertise/ maeneo ya uwezo ya kampuni au watu husika.

g) Ninaagiza NEMC iweke bei elekezi na ukomo kwa *consultants* kwa kila aina ya miradi inayotakiwa kufanyiwa EIA. Hakuna *consultant* ambaye ataenda juu ya bei elekezi katika kundi la miradi husika.

**Mwisho**

Tunaamiini kwamba mabadiliko haya yatatoa mwanzo mpya katika utendaji wa NEMC, hasa katika kusimamia uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira lakini pia uharakishaji wa miradi ya maendeleo na uwekezaji nchini, hasa ujenzi wa viwanda kama azma ya Mheshimiwa Rais wetu inavyoelekeza.

January Makamba (Mb)
Waziri wa Nchi – Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira)
17 Julai 2017